

“RITA KUFANYIA MABORESHO MIFUMO YA USAJILI WA VIFO NA SABABU ZAKE”

Wakala wa usajili ufilisi na udhamini (RITA) unategemea kufanya maboresho ya usajili wa vifo mwanzoni mwa mwezi machi mwaka huu ili kuwezesha upatikanaji wa takwimu sahihi za vifo na sababu zake zitakazosaidia serikali na wadau mbalimbali kuchukua hatua za kukabiliana na sababu hizo.

Serikali kupitia RITA inaendelea na maboresho ya mifumo ya kiteknolojia na sheria ya usajili wa vizazi, vifo, ndoa na talaka katika Mkakati wa kitaifa wa usajili wa matukio muhimu ya Binadamu na ukusanyaji wa takwimu unaojulikana kama National Civil registration and Vital Statistic Strategy (CRVS- Strategy) utakaotoa suluhisho na kukidhi matakwa ya sheria ya usajili wa vizazi, vifo na sababu zake ndoa na talaka kwa kipindi hiki tulichopo. Wakala ulianza na maboresho ya usajili wa vizazi ambapo ulibuni mpango wa kusajili watoto walio na umri chini ya miaka mitano na tayari unaendelea kutekelezwa katika Mikoa tisa hadi sasa ambapo mwezi machi utatekelezwa Mkoa wa Mara na Simiyu.

Akizungumza hii leo Jijini Dar es salaam katika mkutano na wadau kutoka Taasisi mbalimbali za Kitaifa na Kimataifa Mkurugenzi wa Ulinzi wa Haki za Kisheria Bi Lina Msanga amesema mbali na matumizi ya TEHAMA kuwezesha matukio ya usajili wa vifo na sababu zake pia matukio hayo yatasajiliwa pindi tu yanapotokea kwenye Hospitali na Majumbani ambapo vituo vya usajili vitakuwa Ofisi za watendaji kata na vituo vya Tiba.

“kwa sasa takwimu za matukio ya vifo haziridhishi hasa ukizingatia matukio hayo yanaendelea kutokea katika jamii zetu na sote ni mashahidi tunahudhuria katika misiba na hatuoni ndugu au sehemu kifo kilipotokea kufanya jitihada zozote za kusajili labda marehemu akiwa mtu mzima na ameacha mali ndiyo utaona ndugu wanahangaikia kusajili” alisema Bi Msanga.

Maeneo yatakayofanyiwa maboresho kwa upande wa vifo ni mfumo mzima wa kusajili matukio hayo kutoka fomu za karatasi na kuhamia katika teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ambapo simu za mkononi zitatumika kusajili matukio ya vifo na sababu zake kisha taarifa hizo kutumwa moja kwa moja hadi katika Kanzi data ya RITA makao makuu badala ya kutuma fomu zilizojazwa kwa mkono.

Naye mwakilishi kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) Bi Helen Mtove amesema kuwa takwimu za vifo na sababu zake zitawezesha kutoa picha halisi kwa Taifa kwa kuwa na idadi kubwa au ndogo ya wananchi wake wanaopoteza maisha kila siku na hivyo kusaidia kujua sababu na kuchukua hatua ya kukabiliana na tatizo la vifo.

“Mfano tunatambua kuwa Nchi nyingi za kiasia kuna tatizo la vifo vya wanawake wajawazito na watoto chini ya miaka mitano hivyo ni vyema kuwa na takwimu halisi ili kuiwezesha Serikali kuchukua hatua za haraka.” ameeleza Bi Mtove.

Wadau hao waliokutana ni pamoja na Ofisi ya Rais -TAMISEMI, Wizara ya Afya, Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ,Wizara ya katiba na Sheria, Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Shirika la Kimataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) na Benki ya Dunia (WB). Wote kwa pamoja wamependekeza kufanya marekebisho katika fomu za usajili wa vifo zinazotumika kwa sasa huku mifumo na mamlaka nyingine za Serikali zikihimizwa kuwa tayari kushirikiana kwa lengo la kufanikisha maboresho hayo yenye tija kwa Taifa.